| Jina la Mtahiniwa | | Nambari ya Mtahiniwa | |
|---|---|---|---|
| Jina la Shule Yako | | Nambari ya Shule | |
| Sahihi ya Mtahiniwa | | Tarehe | |

**Muda: Saa 1 Dakika 45**

003-2025

# TATHMINI YA SHULE YA JUNIA

## GREDI 8 2025

**JESMA 003**

# - KISWAHILI -

**MAAGIZO WA WATAHINIWA**

1. Andika **jina lako** na **nambari yako ya mtihani** kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
2. Andika **jina** na **nambari ya shule yako** kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
3. Tia sahihi kwenye nafasi uliyoachiwa hapo juu.
4. Andika **tarehe** ya mtihani ipasavyo.
5. Jibu maswali **yote**.
6. Andika majibu **yote** kwa nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki.
7. Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

**MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Sehemu | A | | B | C | D | E | F |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Swali 1 | Swali 2 | Mazungumzo | Sarufi | Fasihi | Novela | Tamthilia |
| Alama ya upeo | | | | | | | |
| Alama ya mtahiniwa | | | | | | | |

**Kijitabu hiki kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

## SEHEMU A: UFAHAMU

**(Alama 5)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi la 5.***

Maisha ya siku hizi ni tofauti sana na yale ya zamani. Mathalani, siku hizi, binadamu halazimiki kufanya kazi za sulubu kama vile kulima, kukoroga zege, kutembea masafa marefu na nyinginezo. Kazi hizi sasa zinatekelezwa na mitambo kwa urahisi haraka na usahihi mkubwa. Isitoshe, kazi ambayo ilihitaji watu wengi kutekeleza sasa inafanywa na mtu mmoja tu ambaye anauongoza mtambo husika pasipo kutoa jasho.

Elimu na maarifa ya kisayansi na teknolojia aidha yamewezesha uvumbuzi wa mbinu bora zaidi za kuongeza kiwango cha chakula kinachozalishwa. Labda ni mataifa yaliyobaki nyuma kimaendeleo tu ambayo yangali yanashindwa kukidhi mahitaji ya raia wake. Uvumbuzi umetuletea mimea ambayo inayostahimili ukame na vimelea huku ikitupatia mazao zaidi. Matokeo yake ni kuwa hata maeneo ambayo hapo awali yalichukuliwa kama yasiyofaa kwa kilimo sasa yanatumika ipasavyo.

Chambilecho wahenga, **hakuna bamvua isiyokuwa na usubi.** Kutegemea sana mitambo kutekeleza shughuli mbalimbali kumechangia uvivu na kuathirika kwa afya ya wengi. Visa vya **maradhi** yanayotokana na mitindo ya maisha navyo vimeongezeka sana. Isitoshe, baadhi ya mimea inayoaminika kuziba pengo la uhaba wa chakula nchini inaingizwa sokoni bila kufanyiwa utafiti wa kutosha: jambo ambalo linaongeza matatizo ya kiafya. Hakika, maendeleo yoyote hufaa zaidi pale ambapo uwajibikaji unapewa kipaumbele.

1. Kwa nini maisha ya siku hizi yamebadilika? Watu
   A. wamekuwa wengi
   B. wamekuwa werevu
   C. hawafanyi kazi zozote
   D. wamerahisishwa maisha na mitambo
2. Jambo lipi **si** sahihi kuhusu mitambo?
   A. Inafanya kazi zote
   B. Inafanya kazi kwa haraka
   C. Inarahisisha kazi ngumu
   D. Inapunguza idadi ya wafanyakazi
3. Mimea iliyovumbuliwa ina sifa zifuatazo isipokuwa,
   A. kustahimili ukame
   B. inakabiliana na vimelea
   C. haihitaji maji
   D. baadhi inaleta madhara
4. Ni maelezo yapi yanaonyesha ukweli wa methali **hakuna bamvua isiyokuwa na usubi?**
   A. Mitambo imerahisisha kazi na kuleta mazao mengi.
   B. Teknolojia ina manufaa mengi lakini inachangia madhara ya kiafya.
   C. Watu hawafanyi kazi lakini wanakidhi mahitaji yao.
   D. Maisha yamekuwa bora lakini si kama zamani.
5. **Kazi za sulubu** kulingana na kifungu hiki ni kazi
   A. nyingi
   B. za lazima
   C. ngumu
   D. za kushirikiana

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 6 hadi la 10.*** **(alama 5)**

Hapo zamani paliishi kijana aliyeitwa Paulo. Kijana huyo alisifiwa sana kwa maarifa yake. Hata hivyo , jambo la kusikitisha ni kwamba alikuwa mzembe kupindukia. Badala ya kufanya kazi, alitamani kukaa nyumbani akitazama runinga au hata kuchezea simu. Ndugu zake wakubwa walimwonya dhidi ya hulka hiyo lakini akatia maskio yake nta.

Siku moja, Paulo alitumwa mtoni akateke maji. Wazo la kubeba chungu chenye maji lilimnyima raha akaanza kusuka mpango wa kuepuka kazi. Alichota maji kidogo kisha akakiangusha chungu kikavunjika vigae vigae huku akipiga kamsa, "Mamba! Mamba! Nisaidieni ! Nafa!....Jamani!". Ndugu zake na majirani walipofika hawakumwona mamba. Paulo alisingizia kuwa mamba amerudi majini.

Ndugu na majirani zake walitikisa vichwa na wakaondoka. Siku nyingine tena alipiga mayowe akiwa shambani kwamba amevamiwa na chui. Ndugu na majirani walikuja tena lakini **matokeo yakawa yale yale;** wakaondoka kwa ghadhabu.

Siku ya tatu, kundi la mbwa mwitu lilijitokeza mbele yake akiwa malishoni. Alipiga mayowe lakini hakuna aliyekuja kumpa msaada. Basi ilibidi apambane sana mpka mbwa mwitu wale wakamwacha. Hata hivyo, alibaki na majeraha makumbwa yaliyomkumbusha kuwa ni wakati wa kukomesha hila zake.

**6.** Ni mambo yapi yanayoonyesha kuwa ndugu walijali maslahi ya Paulo?

A. Kuja mbio kumpa msaada, kumwonya dhidi ya uvivu

B. Kumshirikisha katika kazi, kumwacha achezee simu.

C. Kumpa chungu aende mtoni, kumwonya dhidi ya kuchezea simu

D. Kumhimiza aende shuleni, kumpuuza alipopiga mayowe.

**7.** Paulo alipopiga mayowe siku ya kwanza

A. alikuwa amemwona mamba

B. alikuwa ameingiwa na hofu.

C. ilikuwa njama ya kuepuka kazi

D. ndugu walijua hakuna hatari

**8.** Maneno **matokeo yakawa yale yale** kulingana na kifungu yanaonyesha kuwa,

A. hakuna aliyekuja kusaidia

B. mamba alirudi mtoni

C. chui alitoweka haraka

D. hawakushuhudia hatari yoyote

**9.** Chagua sifa za Paulo kulingana na kifungu hiki.

A. Mwoga, anayependa kutambuliwa.

B. Jasiri asiyependa kufanya kazi.

C. Mvivu, anayepuuza mchango wa wengine

D. Katili, asiyekubali makosa yake.

**10.** Neno **mzembe** kama lilivyotumika katika kifungu hiki lina maana sawa na

A. mjanja B. mvivu

C. mwongo D. mlafi

## MAZUNGUMZO

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu swali la 11 hadi la 15.* (Alama 5)**

**(*Chonde na Sumeya wamekutana sokoni*)**

**Sumeya** : (***Akimnyooshea mkono)*** Waambaje rafiki yangu?

**Chonde** : ______________. Nimekuja sokoni kununua mboga na matunda.

**Sumeya** : Ni muhimu kula mboga na matunda kwa wingi; miili yetu inahitaji vitamini ili kukabiliana na maradhi.

**Chonde** : Sijawahi kukuona ukinunua matunda. Kwani kwenu hamli mboga na matunda?

**Sumeya** : (***Akimwangalia usoni***).Ni kweli sisi huwa hatununui mboga na matunda. Hata hivyo, sisi hula vitamini kwa wingi. Mimi hupanda mboga kama vile sukumawiki, spinachi na kabeji. Pia kwetu kuna miembe, michungwa, ndimu, mipapai na karakara.

**Chonde** : Enhee! Kumbe hiyo ndiyo siri yenu ya kupata mahitaji hayo bila gharama? Nitakuja kwenu unielimishe kuhusu kilimo cha aina hiyo.

**Sumeya** : __15.__, ukija nitakusaidia. Karibu wakati wowote.

***(Wanafika kwa mchuuzi na kuagizia bidhaa mbalimbali )***

**11.** Chagua jibu lifaalo zaidi kujaza pengo la __11__ .
A. Sawa
B. Sijambo.
C. Sina la kuamba
D. Mimi ni mzima

**12.** Ni maelezo yapi yaliyo sahihi kulingana na mazungumzo haya?
A. vitamini huimaisha kinga ya mwili
B. vitamini hujenga mwili
C. vitamini huupa mwili nguvu
D. vitamini haihitajiki sana mwilini

**13.** Hatua alizochukua Sumeya na aila yake ni muhimu kwani,
A. wanauza matunda sokoni na kujiongezea mapato.
B. wanapata mahitaji yao bila kugharamika sana
C. wana mboga na matunda japo hawayahitaji
D. chakula chao ni mboga na matunda pekee

**14.** Mazungumzo hayo yamezingatia kanuni zifuatazo isipokuwa,
A. matumizi yafaayo ya ishara
B. kubadilisha zamu ipasavyo
C. kuitikia kwa viingizi .
D. kukatana kalima katika mazungumzo

**15.** Jaza nafasi ya __15__ kwa kuchagua neno sahihi
A. Hewala
B. Simile
C. Lau
D. Ashakum

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 5)

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 mpaka 20. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jibu lifaalo zaidi.***

Michezo **16.** ______ manufaa mengi **17.** ______ si njia ya **18.** ______ wakati kama wengi wanavyofikiri. Mtu **19.** ______ mazoezi, viungo **20.** ______ hudhoofika kiasi cha kushindwa kujifanyia hata shughuli ndogondogo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **16.** | A. yana | B. zina | C. kuna | D. ina |
| **17.** | A. mingi | B. mengi | C. nyingi | D. jingi |
| **18.** | A. kuvunja | B. kupunja | C. kuvuja | D. kufuja |
| **19.** | A. asipofanya | B. akifanya | C. asivyofanya | D. asiofanya |
| **20.** | A. zake | B. vyake | C. yake | D. wake |

***Jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa***

**21.** Chagua jibu lenye **kiwakilishi cha idadi**.
A. Watoto watatu wanaimba.
B. Wachache wamefika hospitalini
C. Ule ulipandwa na baba yangu
D. Ng'ombe hawa ni wangu

**22.** Jina jingine la mvulana ni
A. ghulamu B. gulamu
C. gashi D. ghashi

**23.** Tambulisha kitenzi kisaidizi katika sentensi ifuatayo;
Nanjala alikuwa akimpikia mwanawe uji wa wimbi
A. wa B. akimpikia
C. uji wa wimbi D. alikuwa

**24.** Andika wingi wa sentensi; **Bawabu alifunga lango hilo**
A. Bawabu wameifunga milango hiyo
B. Mabawabu wameyafunga malango hayo
C. Bawabu wameyafunga malango hayo
D. Mabawabu wameifunga milango hiyo

**25.** Badilisha sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendea
Juma amelifua koti la babu
A. Juma amefulishwa koti la babu
B. Koti la babu limefuliwa na Juma
C. Juma amefulia babu koti
D. Babu amefuliwa koti na Juma

**26.** Kanusha;
Ng'ombe wetu wamepewa chanjo
A. Ng'ombe wetu hawapewi chanjo
B. Ng'ombe wetu hawakupewa chanjo
C. Ng'ombe wetu hawajapewa chanjo
D. Ng'ombe wetu hawatapewa chanjo

**27.** Ni sentensi ipi iliyo katika wakati uliopita hali ya kuendelea
A. Mvua ilikuwa ikinyesha sana
B. Tunatakiwa tukiwaheshimu wazazi
C. Mtoto alikuwa ameshiba
D. Mwalimu alikuja mapema

**28.** **Tajiri** ni kwa **maskini** kama ilivyo **chuki** kwa,
A. wema B. furaha
C. ubaya D. upendo

**29.** Ipi ni nomino ya pekee?
A. Wingu la nzige B. Ziwa Bogoria
C. Huruma D. Barabara

**30.** Andika katika usemi wa taarifa
"Tutafunga shule juma lijalo," mwalimu alisema
A. Mwalimu alisema kuwa tutafunga shule juma lijalo.
B. Mwalimu alisema kuwa watafunga shule juma ambalo lililofuata.
C. Mwalimu alisema kuwa wangefunga shule juma ambalo lingefuata
D. Mwalimu alisema kuwa tungefunga shule juma lijalo

## FASIHI SIMULIZI. (Alama 8)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kwa usahihi.***

Jamii ya Wapawe ilikuwa imestawi sana kupitia kilimo na ufugaji. Mahasimu zao waliingiwa na kinyongo. Mara kwa mara, maadui hao walifanya uvamizi wakaharibu mali na kuwasababishia Wapawe majeraha.

Siku moja, maadui wale walikuja kama kawaida. Walipofika katika mwamba mkubwa uliokuwa karibu na kijiji cha Wapawe, walimkuta shujaa aliyeitwa Ringo akiwa na mkuki mkubwa mkononi. Mkuki huo ulikuwa mrefu hivi kwamba uligusa mawingu. Basi Ringo alizungusha mkuki ule mara moja, ukawafagia wavamizi wale na kuwatupa kilomita kadhaa.

Wapawe walifurahi sana. Walimpa Ringo makazi, mke, mifugo na shamba la kulima. Ikawa kila mara wavamizi walipokuja hata kwa maelfu, Ringo angewapiga dharuba moja ya mkuki wake na kuwatupa mbali sana na mipaka ya kijiji.

Wahenga walisema kuwa hasidi hana sababu. Vijana wachache Wapawe walimwonea wivu Ringo. Walimwendea mkewe kwa ulimi mtamu wakamsaili kuhusu nguvu za miujiza za Ringo. Mke aliwafahamisha kuwa siri ilikuwa pete ya kipekee aliyovalia Ringo akienda vitani. Vijana walifanya njama wakaiba pete ile. Kumbe Ringo mwenyewe alishajua njama yao. Papo hapo alipandwa na hasira kama mkizi kwa usaliti huo. Ngurumo za radi zilisikika kote kukawa na tetemeko la kuogofya. Hata hali ilipotulia, Wapawe hawakumwona Ringo tena.

**31.** **a)** Hadithi hii inaorodheshwa katika kipera kipi cha hadithi? **(Alama 1)**

________________________________________

**b)** Taja sifa **<u>mbili</u>** za hadithi za aina hii ambazo zinadhihirika katika hadithi hii. **(Alama 2)**

**i)** ________________________________________

**ii)** ________________________________________

**c)** Taja vipengele **<u>viwili</u>** ambavyo mtambaji wa hadithi hii anaweza kuzingatia. **(Alama 2)**

**i)** ________________________________________

**ii)** ________________________________________

**d)** Taja shughuli moja ya kiuchumi ambayo jamii ya hadithi hii ilishiriki. **(Alama 1)**

________________________________________

**e)** Hadithi za aina hii ni muhimu sana katika jamii. Toa mifano **<u>miwili</u>** ya umuhimu huo. **(Alama 2)**

**i)** ________________________________________

**ii)** ________________________________________

## NOVELA **(Alama 6)**

***Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Abiria walikuwa wamebanana sisisi. Kalekye alimwona mamake akimpungia mkono kupitia kioo cha dirisha la basi. Alijitahidi kuunyanyua mkono wake aliouhisi mzito kama nanga. Alijitahidi kuzuia machozi yaliyotishia kumdondoka ndondondo akayaficha kwa tabasamu usoni. Tayari alishaanza kuhisi ukiwa wa kuachana na mama yake. Basi liliongeza kasi mama akabaki pale kituoni akiendelea kupunga mkono kumuaga mwanawe wa pekee.

Moyo wa Kalekye ulizidi kumkumbusha mengi. Alikumbuka maisha yake na mamaye pale kijijini tangu kifo cha baba yake miaka mingi iliyopita. Mama alijitahidi akamlea kwa vitanga vya mikono yake hadi hapa alipo msichana mzima. Alikumbuka siku za kulalia mate, kukosa karo, wakati wa fanaka hadi ami yake alipokuja na kumsaidia mamake mzigo wa kumsomesha Kalekye.

Kalekye alikumbuka kuwa jaza ya hisani ni hisani. Alijitahidi kuwa mchwa akifika chuoni ili aonyeshe shukrani kwa mamaye na ami yake kwa juhudi zao. Katu asingekubali shinikizo la rika limpumbaze ajiunge na vijana ambao huasi masomo.

**32.** **a)** Taja mandhari yanayojitokeza katika sehemu hii ya novela. **(Alama 1)**

____________________________________________

**b)** Maudhui ni masuala ambayo mwandishi hushughulikia katika kazi ya fasihi. Jadili suala **<u>moja</u>** lililoshughulikiwa katika sehemu hii ya novela. **(Alama 2)**

____________________________________________

____________________________________________

**c)** Taja sifa moja ya Kalekye inayojitokeza katika sehemu hii ya novela. **(Alama 1)**

____________________________________________

**d)** Huku ukitolea mifano ifaayo, eleza vipengele **<u>viwili</u>** vya lugha ambavyo vimetumiwa kuwasilisha ujumbe katika sehemu hii ya novela. **(Alama 2)**

**i)** ________________________________________

**ii)** ________________________________________

## TAMTHILIA **(Alama 6)**

***Soma sehemu ifuatayo ya tamthilia kisha ujibu maswali uliyopewa.***

***Sehemu ya I***

***Onyesho la I***

***(Bwana Omari amekaa mezani. Mwanawe, Yohana anafika huku amebeba chupa ya chai moto. Anammiminia babaye kisha anaketi.***

**Yohana** : Shikamoo baba! Karibu chai.

**Bwana Omari** : *(Akimwangalia mwanawe)* Marahaba. Asante kwa chai.

**Yohana** : Karibu. *(Ananyamaza kidogo)* Baba, ulisema kuwa unataka kuniona. Je, una lipi?

**Bwana Omari** : *(Kwa utulivu)* Mjomba wako amenipigia simu kutoka mjini.

**Yohana** : *(Kwa furaha)* Hali iko vipi, barua yangu ya kuomba kazi imejibiwa?

**Bwana Omari** : Bado..... bado hajapata jibu. Hata hivyo alikuwa na pendekezo jingine.

**Yohana** : Ooh! Nilidhani nimebahatika kama mtende kumbe habari ni za kutamausha?

**Bwana Omari** : *(Akimgusa mkono)* Mwanangu, wajua kazi mbi si mchezo mwema. Ingawa una shahada ya chuo kikuu, kazi zimeadimika mithili ya wali wa daku. Tena wajua mimi baba yako sina chochote cha kusema vizuri na wazee.

**Yohana** : Usijali baba. Hongo ni haramu. Sitaki mtu yeyote atoe mlungula ili nipate kazi. Hakika, kazi ya aina hiyo haitanipa utulivu wa moyo.

**Bwana Omari** : Mjomba wako anapendekeza ufanye kazi ya utarishi katika kampuni anayofanya kazi ukisubiri milango ya heri ifunguke.

**Yohana** : Hayo ni sawa baba. Najua mjomba Saleh ni mja mwenye mkono wazi. Bila shaka ataendelea kunisaidia.

**Bwana Omari** : Kesho tutafanya maandalizi. Mjomba wako atakuja kukuchukua kesho kutwa uandamane naye mjini.

**a)** Eleza sifa **mbili** za tamthilia zinazojitokeza katika sehemu hii ya tamthilia.

**(Alama 2)**

i) ______________________________

ii) ______________________________

**b)** Jadili suala lolote lililoshughulikiwa katika sehemu hii ya tamthilia. **(Alama 2)**

______________________________

______________________________

**c)** Maelezo yaliyofungiwa katika mabano huitwaje? **(Alama 2)**

______________________________

______________________________

**d)** Taja sifa **moja** ya Yohana kulingana na sehemu hii ya tamthilia. **(Alama 1)**

______________________________

JESMA 003

# TATHMINI YA AWAMU AWALIA
# GREDI YA NANE 2025
# - INSHA -

003-2025

**Muda: Dakika 40**

**Jina la mwanafunzi:** ........................................................ **Nambari ya Tathmini:** ..................

**Shule:** ........................................................................... **Gredi 8:**................ **Tarehe:** ......................

*Mwandikie rafiki yako barua ukimshukuru kwa kukutembelea katika likizo iliyopita.* **(alama 20)**


Tovuti: www.jesmapublishersltd.com Baruapepe: jesmapublishers@yahoo.com
©Jesma Publishers & Educational Boosters Ltd.Simu: 0794677748/0701545759
WARNING: It is an offence to ...